NANI KAMA CCM?

Nani kama CCM? Vyama vya Siasa vipo vingi kama utitiri. Viko vinavyochechemea. Vipo vinavyojikongoja. Vipo vilivyo katika sakratmauti. Chama pekee chenye uhai, afya, utomvu wa uzima na karisima; ni Chama Cha Mapinduzi tu. Kilinganishe CCM na genge la vyama vingine. Tofauti ipo kubwa. Chama Cha Mapinduzi kinapishana na vyama vya wapinzani kwa masafa makubwa, kama mbingu na ardhi. Mwendo wa CCM ni mkubwa na wa kazi na daima unapishana na ule wa kambi ya upinzani wa kuchechemea. Sababu zipo nyingi juu ya tofauti hii. Chama Cha Mapinduzi ni chama **makini**. Hakuna migogoro. Hakunga ngwara, kutoana ngeu wala mieleka huko. Viongozi hawatoani macho kwa kugombea ruzuku. **Udini**, **ukabila** au **umimi** ni mambo yasiyoendekezwa kama yalivyo kwa vyama vingine. Hiki CCM ni chama pekee chenye uzoefu wa kuongoza nchi na watu. Hatima ya maisha ya Watanzania yamo mikononi mwa viongozi hawa waadilifu na wanachama wa Chama hiki. CCM kama mtoto wa ASP na TANU, waliongoza watu wa nchi hii kudai uhuru kutoka kwa Wakoloni wa Kiingereza kwa Tanzania Bara na Usultani na ukoloni wa Kiingereza kwa Tanzania Zanzibar. Kazi hii ya ASP na TANU ya kuikomboa Zanzibar na Tanganyika, inaipa heshima na nafasi adhimu CCM kwa wakati wote. Vyama vya upinzani havikuwepo wakati huo wa mapambano, kwa hivyo leo havina nafasi ya kupewa uongozi kwani havina historia. Havijui machungu ya kutawaliwa. Wengi wa viongozi wake ni watoto. Baada ya Uhuru na Mapinduzi, ASP na TANU vikafanya mambo makubwa ya kurejeshea heshima Watanzania iliyonyimwa na uovu wa ukoloni na Usultani. TANU, ASP na baadaye CCM, viliendelea kuwaondolea shida, tabu na kero za wananchi wa nchi hii. Uzoefu wenye tija na manufaa wa waasisi hao na wa Taifa hili, Nyerere na Karume, umerithiwa na viongozi wa sasa wa Chama Cha Mapinduzi. Viongozi hao wanaofata nyayo za waasisi hawa ndio wanaoongoza Serikali zetu kw aufanisi mkubwa. Watanzania ni watu wenye busara na hekima. Hakuna atakayekubali kuongozwa na viongozi vichanga visivyokomaa ambao wasiowahi kuongoza hata Serikali ya Kitongoji. Uongozi wa nchi hii sio wa kujifunzia. Taifa letu haliwezi kufanyiwa majaribio. Viongozi wengi wa vyama vya upinzani ni wale walioshindwa maisha. Chama Cha Mapinduzi ndicho chenye hazina na dafina ya **viongozi bora**. Hivyo kuchagua viongozi wa kuongoza Serikali za Mitaa, Vijiji au Vitongoji miongoni mwao wapinzani ni kupoteza muda bure. Viongozi wao wote hawana sifa za msingi za kuwa kiongozi bora. Wananchi wasighilibike wakadhani upinzani kama "maziwa ya mgando", hapana hayo ni matapishi, wananchi katu wasifakamiye watadhurika. Ashakum, mtaharisha! Watanzania wasisahau wosia wa Mwalimu Nyerere pale aliposema "**kiongozi bora atatoka ndani ya CCM**" Chama Cha Mapinduzi **hakina udikteta**. Wagombea huchaguana kwa njia ya demokrasia. Hakuna mizengwe, hakuna ukabila au udini. Kwa vile chama cha CCM hakina udikiteta taabani na Serikali zake zitaimarisha utawala bora na kuheshimu haki za binadamu. Huko katika kambi ya upinzani ni vurugu mechi. Umejaa **umimi**. Wagombea wao hawachaguliwi bali huichagua au kujiteua. Wengine viongozi huwapa nafasi jamaa yake, mke wake, shemeji yake au hawara yake. Toba! Chama Cha Mapiduzi kina **sera safi** zinazotekelezeka. Hivi sasa rekodi ya ufanisi ni kubwa sana. Ni rekodi ambayo haikuwahi kufikiwa tangu Tanzania ilipoumbwa. Hakuna eneo lisilokuwa na mafanikio ya kupigiwa mfano kimaendeleo. Sekta ya uchumi imepiga hatua tokea kukua kwa uchumi, kushuka kwa mfumko wa bei, kuongezeka kwa akiba ya fedha za kigei na kuongezeka kwa mapato ya kila mwezi. Nani anabishia hilo? Sekta ya elimu yapo mengi ya chama hiki ya kujivunia kwa Serikali yake. Ongezeko la Shule za Msingi, Sekondari, Vyuo, Vyuo Vikuu, ujenzi wa madarasapamoja na ongezeko la walimu na kadha wa kadha. Karo ya shule za Sekondari imepunguzwa. Huduma za Afya zimeboreka kwa kufikia kiwango cha kimataifa cha asilimia 90% ya chanjo, ongezeko la vituo vya afya, zahanati, hospital na kuwekwa mashine za 'Xray', 'Ultrasound' katika hospital nyingi; "wenye macho wanayaona!" Serikali itaokoa maisha ya watu wengi kwa kutoa bure dawa za kuefusha maisha za ukimwi. Serikali ipewe heko. Huduma za maji, mabwawa na malambo pia zieimarishwa. Sera za chama hiki zimeondoa kero sugu zakodi katika Halmashauri, Mitaa na Vijiji. Lakini kubwa kuliko yote, Chama Cha Mapinduzi kinajivunia sana kuweka nchi hii kuwa ya **Amani**. Nchi yenye umoja wa ajabu na upendo usiomithilika. Waswahili husema "**usione vyaelea vimeundwa**". Naam! Hivyo, nani hajui mazuri yote haya ya kimaendeleo, **usitawi**, **umoja** na **amani** yameletwa na Chama Cha Mapinduzi kilicho makini? Chama chenye Viongozi **razin** na wenye **hekima** na **busara**. Chama chenye **Sera safi** na **bora**. Watanzania msifanye makosa katika uchaguzi wa Serikali za **Mitaa**, **Vijiji** na **Vitongoji**. Chagueni viongozi kutoka Chama Cha Mapinduzi. Mwaka 1994 Watanzania walichagua CCM kwa kishindo cha asilimia 95% katika chaguzi za Mitaa, Vijiji na Vitongoji. Mema na mafanikio hayo yote ni kuipa kura nyingi CCM. Kumbe ilikuwa uamuzi wa busara. Mwaka huu wapinzani pia wabaneni mbavu. Wembe uwe kuliko ule Wapinzani wanyolewe bila vichwa kutiwa maji. Ushindi uwe wa kishindo. **Nani kama CCM? H A K U N A !** .

muhammedkhatib@yahoo.co.uk